KANISA KATOLIKI -TANZANIA

SHIRIKA LA ROZARI HAI ULIMWENGUNI.

ROZARI HAI MTANDAONI TANZANIA.



# NOVENA KWA BIKIRA MARIA MKINGIWA DHAMBI YA ASILI: 29 Novemba- 07 Desemba 2021

*(Sikukuu ya Bikira Maria mkingiwa dhambi ya asili – 08 Desemba)*

*(Novena hii ina sehemu i-v kila siku)*

***I .Kwa jina la Baba na la Mwana na Roho Mtakatifu, Amina.***

***Sali sala ya Kutubu….***

***Sala ya kumwalika Roho Mtakatifu***

*Uje Roho mtakatifu, uzienee nyoyo za waumini wako, peleka roho wako, vitaumbwa upya na utaufanya uso wa dunia uwe mpya.*

***Tuombe:***

*Ee Mungu, unayefundisha mioyo ya waumini wako, ukiwaletea mwanga wa Roho Mtakatifu, tunaomba utujalie kwa msaada wa Roho huyo kutambua yanayofaa na kufurahia daima faraja zake. Amina.*

Kila siku ya novena anza na sala ifuatayo kwa Bikira Maria mkingiwa dhambi ya asili, kisha Sali sala ya siku husika na kumalizia kwa litania ya Bikira Maria.

## II NIA ZA NOVENA

**1.Kuliombea Kanisa Takatifu la Mungu na Viongozi wa Kanisa**

**2.Kuombea wongofu wa Wakosefu**

**3. Kuomba tupate mvua za kutosha kuepukana na njaa na ukame.**

**4. Kuombea Ufanisi wa Mafungo ya Majilio.**

**5. NIA BINAFSI PAMOJA NA KUOMBEA ROHO TESEKA TOHARANI ZIOKOKE KWA NJIA YA MARIA.**

## III. Sala kwa Bikira Maria mkingiwa Dhambi ya Asili

Ee Mungu, ambaye kwa kukingiwa dhambi ya asili kwa Bikira Maria mwenyeheri, ulitayarisha makao yanayostahili ya kuishi mwanao, tunakuomba kama ambavyo kwa matarajio ya kuzaliwa na kifo cha mwanao, ulimlinda Bikira Maria dhidi ya madoa yote, uruhusu tena tusafishwe na

kwa maombezi yake, utufikishe kwako, kwa njia ya Bwana wetu Yesu Kristo, mwanao,anayeishi na kutawala daima nawe katika umoja wa Roho Mt.Mungu daima na milele. Amina.

**Siku ya kwanza:**

Ee Bikira Mt. sana, uliyempendeza Mungu, uliye mama yake, mkingiwa dhambi ya asili katika mwili na roho, kwa Imani na mapendo, ninakuomba uniangalie kwa wema mimi ninayekuomba msaada. Ee mama Mt. sana, ambaye kwa kukingiwa dhambi ya asili, ulikanyaga kichwa cha adui wako pale ulipochukua mimba, tunaomba uzipokee sala zetu uyafikishe katika kiti chako cha enzi cha Mungu maombi yetu….(taja hitaji lako) Ee Maria mkingiwa dhambi ya asili, Mama wa Kristo,uliyependwa na kusikilizwa na mwanao mpendwa ulipokuwa hapa duniani na hata sasa huko mbinguni ulipo,tunakuomba utuombee na kutupatia kutoka kwake, mahitaji yetu tunayokuomba, kama ni mapenzi ya Mungu. Amina **Litania ya Bikira Maria……………..**

**Siku ya Pili:**

Ee Maria, Bikira Mwenyeheri daima, mama wa Mungu, Malkia wa malaika na wote, tunapotafakari kukingiwa kwako dhambi ya asili, tunakusalimu kwa heshima kubwa sana. Tunakushukuru kwa ulinzi wako wa kimama na kwa Baraka nyingi ambazo tumezipata kwa maombezi na huruma zako. Katika mahitaji yetu yote, tunakukimbilia tukiwa na matumaini thabiti. Ee mama wa huruma, tunakuomba uyasikilize maombi yetu sasa na kutupatia kutoka kwa mwanao hitaji letu tunaloliomba kwa bidii sana katika novena hii……(taja hitaji lako) Ee Maria mkingiwa dhambi ya asili, Mama wa Kristo, uliyependwa na kusikilizwa na mwanao mpendwa ulipokuwa hapa duniani na hata sasa huko Mbinguni ulipo, tunakuomba utuombee na kutupatia kutoka kwake, mahitaji yetu tunayokuomba, kama ni mapenzi ya Mungu. Amina.
**Litania ya Bikira Maria………..**

**Siku ya Tatu:**

Ee Bikira Maria mwenyeheri, utukufu wa wakristo, furaha ya kanisa na mama wa Bwana wetu, utuombee katika Moyo wa Yesu, ambaye ni mwanao na kaka yetu. Ee Maria, ambaye kwa kukingiwa dhambi ya asili ulikuja duniani bila doa, kwa huruma yako utuombee kwa Yesu atujalie hitaji hili la pekee tunaloliomba kwa bidii……..(taja hitaji lako) Ee Maria mkingiwa dhambi ya asili, Mama wa Kristo, uliyependwa na kisikilizwa na mwanao mpendwa ulipokuwa hapa duniani na hata sasa huko mbinguni ulipo, tunakuomba utuombee na kutupatia kutoka kwake, mahitaji yetu tunayokuomba, kama ni mapenzi ya Mungu. Amina.
**Litania ya Bikira Maria……………**

**Siku ya Nne:**

Ee Maria, Mama wa Mungu, uliyekingiwa dhambi ya asili, ulikuwa umejaa neema za pekee kati ya wanawake wote, kwa kuwa ni mama na bikira; Mama na Bikira wa Kristo, tunakuomba kutoka katika kiti chako cha enzi, utuangalie kwa moyo wako wenye huruma na kusikiliza sala zetu, tunakuomba utupatie ombi letu tunalolileta kwako sasa……….(taja hitaji lako). Ee Maria mkingiwa dhambi ya asili, Mama wa Kristo,uliyependwa na kusikilizwa na mwanao mpendwa ulipokuwa hapa duniani na hata sasa huko mbinguni ulipo, tunakuomba utuombee na kutupatia kutoka kwake, mahitaji yetu tunayokuomba, kama na mapenzi ya Mungu. Amina.

**Litania ya Bikira Maria………….**

**Siku ya Tano:**

Ee Mungu, ambaye kwa kukingiwa dhambi ya asili kwa Bikira Maria mwenyeheri, ulitayarisha makao yanayostahili ya kuishi mwanao, tunakuomba kama ambavyo kwa matarajio ya kifo cha mwanao, ulimlinda Bikira Maria dhidi ya madoa yote, utujalie kwa maombezi yake, tupate neema tunazoziomba sasa…(taja hitaji lako) Ee Maria mkingiwa dhambi ya asili, Mama wa Kristo, ulipendwa kwa kusikilizwa na mwanao mpendwa ulipokuwa hapa duniani na hata sasa huko mbinguni ulipo,tunakuomba utuombee na kutupatia kutoka kwake, mahitaji yetu tunayokuomba, kama ni mapenzi ya Mungu. Amina.

**Litania ya Bikira Maria………**

**Siku ya Sita:**

Malkia wa mbinguni mtukufu na wa milele, tunasadiki kwa uthabiti kukingiwa kwako dhambi ya asili kulikofanywa kwa ajili ya mwanao. Tunafurahi pamoja nawe katika kukingiwa kwako dhambi ya asili. Tunamshukuru Mungu mmoja anayetawala milele katika nafsi tatu, Baba, Mwana na Roho Mtakatifu kwa kukingiwa kwako dhambi ya asili. Ee mama wa neno aliyejifanya mtu, ulisikilize ombi letu tunalokuomba kwa namna ya pekee katika novena hii…….(taja hitaji lako) Ee Maria mkingiwa dhambi ya asili, Mama wa Kristo, uliyependwa na kusikilizwa na mwanao mpendwa ulipokuwa hapa duniani na hata sasa huko mbinguni ulipo, tunakuomba utuombee na kutupatia kutoka kwake, mahitaji yetu tunayokuomba, kama ni mapenzi ya Mungu. Amina.

**Litania ya Bikira Maria………….**

**Siku ya Saba:**

Ee Bikira, mkingiwa dhambi ya asili, Mama wa Mungu na Mama yangu, kutoka katika kilindi cha heshima na utukufu wako uniangalie kwa macho yako yenye huruma, mimi niliye na matumaini kamili kwa wema wako, ninayesadiki kukingiwa kwako dhambi ya asili na ninayefahamu vema uwezo wako. Ninakuomba uje kutusaidia na umwambie mwanao atujalie neema tunayoiomba kwa bidii katika novena hii, iwapo kama ni kwa ajili ya roho zetu na roho za wale tunaowaombea………..(taja hitaji lako) Ee Maria mkingiwa dhambi ya asili, Mama wa Kristo, uliyependwa na kusikilizwa na mwanao mpendwa ulipokuwa hapa duniani na hata sasa huko mbinguni ulipo, tunakuomba utuombee na kutupatia kutoka kwake, mahitaji yetu tunayokuomba, kama ni mapenzi ya Mungu. Amina.

**Litania ya Bikira Maria……………..**

**Siku ya Nane:**

Ee Bikira Maria mwenye neema nyingi sana, mama mpendwa wa Yesu kristo, mwokozi wetu, utuombee kwake ili tujaliwe neema tunayoiomba kwa bidii katika novena hii……..(taja hitaji lako) Ee mama wa neno aliyefanyika mwili tunapata nguvu tukiamini kwamba sala zako kwa ajili yetu zinasikilizwa kwa wema katika kiti cha enzi cha Mungu, Ee mtukufu mama wa Mungu, kwa ukumbusho wa kukingiwa kwako dhambi ya asili, uyasikilize maombi yetu na kutupatia mahitaji yetu, tunayoyaleta kwako. Ee Maria mkingiwa dhambi ya asili, Mama wa Kristo, uliyependwa na

kusikilizwa na mwanao mpendwa ulipokuwa hapa duniani na hata sasa huko Mbinguni ulipo, tunakuomba utuombee na kutupatia kutoka kwake, mahitaji yetu tunayokuomba, kama ni mapenzi ya Mungu. Amina.

**Litania ya Bikira Maria………………..**

**Siku ya Tisa:**

Ee Mama wa mfalme wa dunia, binadamu mkamilifu kuliko wote, tunakukimbilia wewe kama Mama yetu, mwombezi na mpatanishi wetu. Ee Maria Mt; kwa kukingiwa kwako dhambi ya asili utusaidie katika hitaji letu la sasa. Ee Maria uliyekingiwa dhambi ya asili, tunakuomba kutoka katika vilindi vya mioyo yetu, utuombee kwa mwanao tujaliwe neema hii tunayoiomba……(taja hitaji lako) Ee Maria mkingiwa dhambi ya asili, Mama wa Kristo, uliyependwa na kusikilizwa na mwanao mpendwa ulipokuwa hapa duniani na hata sasa huko mbinguni ulipo, tunakuomba utuombee na kutupatia kutoka kwake, mahitaji yetu tunayokuomba, kama ni mapenzi ya Mungu. Amina.

**Litania ya Bikira Maria……………….**

**IV. TUNAKIMBILIA ULINZI WAKO.**

**Kwa jina la Baba na la Mwana na la Roho Mtakatifu, Amina.**

**V. WIMBO:  BIKIRA MARIA MAMA WA MUNGU KWELI**

**/Bikira Maria  Mama wa Mungu kweli, ulizaliwa pasipokuwa na dhambi x2/**

1. Hakuna mwanamke mwingine duniani, aliyebarikiwa kama ulivyo, twakusifu tunakuheshimu.

2. Malaika mbinguni wasifu jina lako, na duniani kote tunalitaja, utamu wa jina hauishi.

3. Sifa zako zavuma popote duniani, jinalo twalitaja tukitetemeka, njoo kwetu uishi na sisi.

4. Twataka kukuona lakini hatuwezi, kwa kuwa tu wanyonge na wenye dhambi, uzisikilize sala zetu.

********************************AVE MARIA**********************************

**NA: FORTUNATA R.W.MASAKA.**
**MRATIBU ROZARI HAI-MTANDAONI.(0717 558222)**

**rozarihaitanzania@gmail.com**

**www.rozarihai.or.tz**